## CALL FOR INNOVATION SUPPORT PROGRAM

### Opportunity for Setting up and Piloting Water, Sanitation and Hygiene (WASH) Innovative Cluster Initiatives

The Tanzania Women Chamber of Commerce (TWCC), the apex body for women's economic empowerment established in 2005, invites innovators, entrepreneurs, and/or SMEs to join a transformative journey in the formation of Water, Sanitation, and Hygiene (WASH) cluster in Manyara. As the umbrella organization representing women in business across Tanzania, TWCC has consistently championed growth through advocacy, training, mentorship, market linkages, and financial services. Building on this foundation, TWCC is implementing this Innovative Cluster on behalf of COSTECH, in collaboration with UNICEF, applying the Triple Helix model to foster collaboration between academia, entrepreneurs, and government authorities. This initiative empowers entrepreneurs to leverage science and technology from research and higher education institutions, while engaging government stakeholders to co-create sustainable solutions in WASH challenges through the BSF Technology. Guided by five innovative cluster principles, the program seeks to catalyze scalable, resilient, and inclusive innovations that utilizes the BlackSoldier Fly Technology, that will not only address immediate sectoral needs but also strengthen Tanzania's innovation ecosystem. Through this call, TWCC invites visionary thinkers and practitioners to contribute to shaping a cleaner, healthier, and more sustainable future.

This call is therefore seeking companies/individuals working in WASH or are interested in developing the WASH value chain, and to establish a cluster. The proposed WASH Cluster will be established in Manyara region given the relative connectivity that the region offers in the north circuit, with connectivity to Arusha, Mara, Dodoma and Singida.

### Objectives of the WASH Cluster

- Technology transfer of the Black-Soldier-Fly Technology to Manyara
- Foster collaboration among WASH value chain actors.
- Promote innovation and the adoption of sustainable technologies.
- Improve efficiency, market access, and value addition; and

- Support environmental sustainability and green job creation.

**Target Areas**

Interested applicants may be involved in, but not limited to:

- Waste collection, sorting and transportation
- Recycling and upcycling (plastics, paper, metals, glass, e-waste, organic waste)
- Composting and organic waste processing
- Waste-to-energy and resource recovery technologies
- Innovative waste management technologies, products or services
- Environmental sanitation and circular economy solutions

**Eligibility**

The call is open to all women who are members of TWCC, and are located in Manyara or nearby regions. Applicants should be;

1. Individuals, Registered or unregistered SMEs with innovative ideas, technical skills, or entrepreneurial interests, operating or intending to operate within the WASH sector.
2. Businesses that have already established products and clients, but need support in achieving significant growth or in reaching regional and international markets.
3. Residents or operate their business in Manyara and are willing to collaborate and work collectively with other upcoming cluster members.
4. Committed to participate in capacity building, innovation processes and all innovative cluster development initiatives including the implementation of the five guidelines for innovative cluster.
5. Recognized BSF as a pilot technology for animal feed production that supports WASH by converting organic waste into protein, while also producing valuable by-products such as composite fertilizers, thereby contributing to circular economy practices and environmental sustainability.

**Submission Requirements**

Interested applicants are requested to submit

1. A dully filled application form
2. Brief description of current activities, experience or innovation idea; and area of interest in WASH value chain (1 page)
3. Motivation for joining the Waste Management Innovative Cluster (1 page)
4. Copy of ID and any relevant certificates to support her application

**Funding type**

Successful applicants will not receive direct financial grants or monetary awards. Instead, the project will provide comprehensive technical support, including guidance, resources, and expertise, to help participants effectively develop and implement their proposed initiatives.

**Fundable activities for this supporting scheme**

- Initial product, process (comprehensive technology package) and prototype development;
- Sourcing of intellectual property opinions/assets;
- Production of market samples and/or associated testing;
- Refining and implementing designs;
- Conducting field studies to test the assumptions made about the technology, market and/or customer needs;
- Support of certification activities and specification sheet development;
- Piloting, and technology scale-up;
- Techno-economic evaluation studies;
- Detailed primary market research;
- Business plan development.

**Non-fundable activities include**

- Salary contributions to the cluster members or leaders
- Infrastructure (i.e. Equipment and building) except for specialized equipment that is within the budget constraints and required to enable qualifying activities.
- Early-stage research projects;
- Student bursaries, research projects and extended periods of work

**Call Opening:** 15th April 2026

**Submission deadline**: 30th April, 2026 at 11:59 PM

All Applications should be submitted via emails at info@twcc-tz.org or through postal address at Executive Director, TWCC, P.O. Box 5591, Dar-es-Salaam.

For further information/ inquiries contact Mr. Nelson Clavery through +255756565381 or nelsonclevery@twcc-tz.org OR Dr. Prosper Massawe through +255764629793 or prosper.massawe@costech.or.tz

**Language**

Applications can be submitted in English or in Kiswahili.

**WITO WA MPANGO WA KUUNGA MKONO UBUNIFU**

**Fursa ya Kuanzisha Kongano la Ubunifu katika Sekta ya Maji, Usafi na Usafi wa Mazingira (WASH)**

**Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC)**, chombo kikuu cha uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake kilichoanzishwa mwaka 2005, kinawaalika wabunifu, vikundi na wajasiriamali kushiriki katika safari ya mabadiliko ya kuanzisha **Kongano la Ubunifu katika WASH** mkoani Manyara. Kama mwavuli wa wanawake wafanyabiashara nchini Tanzania, TWCC imekuwa ikihimiza ukuaji kupitia utetezi, mafunzo, ushauri, uunganishaji wa masoko na huduma za kifedha. Tukijenga juu ya msingi huu, TWCC inatekeleza **Kongano Bunifu** kwa niaba ya COSTECH, kwa kushirikiana na UNICEF, kwa kutumia **mfumo wa Triple Helix** unaohusisha ushirikiano kati ya vyuo vikuu, wajasiriamali na mamlaka za serikali. Mpango huu unawawezesha wajasiriamali kutumia sayansi na teknolojia kutoka taasisi za utafiti na elimu ya juu, huku ukihusisha wadau wa serikali kuunda suluhisho endelevu kwa changamoto za WASH kupitia **Teknolojia ya Black Soldier Fly (BSF)**. Tukiongozwa na kanuni tano za Kongano bunifu, mpango huu unalenga kuchochea ubunifu unaoweza kupanuka, kustahimili na kujumuisha, unaotumia teknolojia ya BSF si tu kutatua mahitaji ya haraka ya sekta bali pia kuimarisha ekosistemu ya ubunifu nchini Tanzania. Kupitia wito huu, TWCC inawaalika wabunifu na watendaji wenye maono kushiriki katika kuunda mustakabali safi, wenye afya na endelevu.

**Malengo ya Kongano la WASH**

- Kuhaulisha Teknolojia ya Black Soldier Fly kwenda Manyara
- Kukuza ushirikiano miongoni mwa wadau wa sekta ya WASH
- Kukuza ubunifu na matumizi ya teknolojia endelevu
- Kuboresha ufanisi, upatikanaji wa masoko na kuongeza thamani
- Kusaidia uendelevu wa mazingira na uundaji wa ajira za kijani

**Maeneo Lengwa**

Waombaji wanaweza kushiriki katika, lakini siyo tu:

- Ukusanyaji, uchambuzi na usafirishaji wa taka
- Uchakataji na uboreshaji wa taka (plastiki, karatasi, chuma, glasi, taka za kielektroniki, taka za kikorganic)
- Utengenezaji wa mbolea na uchakataji wa taka za kikorganic
- Teknolojia za taka kuwa nishati na urejelezaji rasilimali
- Bidhaa au huduma bunifu za usimamizi wa taka
- Usafi wa mazingira na suluhisho za uchumi mzunguko

**Vigezo vya Ustahiki**

Wito huu uko wazi kwa wanawake wote wanachama wa TWCC walioko Manyara au mikoa

jirani. Waombaji wanapaswa kuwa:

- Watu binafsi, vikundi, SMEs zilizosajiliwa au zisizosajiliwa zenye mawazo bunifu, ujuzi wa kiufundi au nia ya ujasiriamali katika sekta ya WASH
- Biashara zilizo na bidhaa na wateja tayari, lakini zinahitaji msaada kufikia ukuaji mkubwa au masoko ya kikanda na kimataifa
- Wakazi wa Manyara au wanaoendesha biashara zao Manyara na wako tayari kushirikiana na wanachama wengine wa cluster
- Wenye dhamira ya kushiriki katika kujenga uwezo, michakato ya ubunifu na utekelezaji wa kanuni tano za cluster za ubunifu
- Wakitambua BSF kama teknolojia ya majaribio ya uzalishaji wa chakula cha mifugo inayosaidia WASH kwa kubadilisha taka za kikorganic kuwa protini na kuzalisha bidhaa zenye thamani kama mbolea mchanganyiko, hivyo kuchangia katika uchumi mzunguko na uendelevu wa mazingira

**Mahitaji ya Uwasilishaji**

Waombaji wanatakiwa kuwasilisha:

- Fomu ya maombi iliyojazwa kikamilifu
- Maelezo mafupi ya shughuli za sasa, uzoefu au wazo la ubunifu na eneo la maslahi katika mnyororo wa thamani wa WASH (ukurasa 1)
- Motisha ya kujiunga na Kongano katika maeneo ikijumuisha Usimamizi wa Taka (ukurasa 1)
- Nakala ya kitambulisho na vyeti husika vinavyounga mkono maombi

**Aina ya Ufadhili**

Waombaji watakaofanikiwa hawatapata ruzuku ya moja kwa moja au zawadi za kifedha. Badala yake, mradi utatoa msaada wa kiufundi wa kina, ikiwemo mwongozo, rasilimali na utaalamu, kusaidia washiriki kuendeleza na kutekeleza ipasavyo miradi yao.

**Shughuli Zitakazofadhiliwa**

- Uendelezaji wa bidhaa za awali, mchakato (pakiti kamili ya teknolojia) na prototaipu
- Upatikanaji wa maoni/rasilimali za mali miliki
- Uzalishaji wa sampuli za soko na/au majaribio husika
- Uboreshaji na utekelezaji wa miundo
- Utafiti wa shambani kuthibitisha dhana kuhusu teknolojia, soko na/au mahitaji ya wateja
- Msaada wa shughuli za uthibitishaji na utayarishaji wa karatasi za viwango
- Majaribio na upanuzi wa teknolojia
- Tafiti za tathmini ya kiuchumi na kiteknolojia
- Utafiti wa kina wa soko la msingi
- Uendelezaji wa mpango wa biashara

**Shughuli Zisizofadhiliwa**

- Mchango wa mishahara kwa wanachama au viongozi wa cluster

- Miundombinu (vifaa na majengo) isipokuwa vifaa maalum vilivyo ndani ya bajeti na vinavyohitajika kuwezesha shughuli zinazostahiki
- Miradi ya utafiti wa awali
- Ruzuku za wanafunzi, miradi ya utafiti na vipindi virefu vya kazi

**Ufunguzi wa Wito: 15 Aprili 2026**
**Mwisho wa Uwasilishaji: 30 Aprili 2026 saa 5:59 usiku**

Maombi yote yawasilishwe kupitia barua pepe: **info@twcc-tz.org** au kwa posta: **Mkurugenzi Mtendaji, TWCC, S.L.P. 5591, Dar-es-Salaam**.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

- **Bw. Nelson Clavery** kupitia +255756565381 au nelsonclevery@twcc-tz.org
- **Dkt. Prosper Massawe** kupitia +255764629793 au prosper.massawe@costech.or.tz

**Lugha**

Maombi yanaweza kuwasilishwa kwa **Kiingereza** au **Kiswahili**.